Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

# SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi

Ifanye haki

Iwe shauku

Toleo Na. 006 | Jarida la kila miezi mitatu | Aprili - Juni, 2011

# Mahkama Zaombwa Kusaidia Maslahi ya Mtoto

**MAJAJI**, mahakimu na makadhi wamefanyiwa semina ya kujadili njia bora za kusaidia kutetea haki za watoto kwa kuyapa kipaumbele maslahi ya mtoto (*best interests of the child*).

Semina hiyo iliandaliwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kwa kushirikiana na Save the Children na uongozi wa Mahkama Zanzibar.

Wataalamu wa sheria kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walijadiliana njia bora za kusaidia maslahi ya watoto ambao haki zao zinavunjwa na watoto wanaokinzana na sheria.

Aidha, washiriki walielezwa kuhusu ongezeko la kesi za ubakaji kwa watoto lakini misingi ya taratibu za Sheria hususan sheria ya ushahidi imekuwa ni kikwazo kwa wahusika kutiwa hatiani na kupewa adhabu.

Kutotiwa hatiani na kuadhibiwa kwa washtakiwa wa kesi za kubaka kumeongeza kasi ya ongezeko la kesi za kubaka Zanzibar.

Jumla ya mada sita ziliwasilishwa katika semina hiyo ya siku mbili iliyofanyika katika Grand Palace Hotel iliopo

Inaendelea Uk. 3



*Mrajis wa Mahkama Kuu Zanzibar, Bw. George Kazi akimtambulisha mgeni rasmi Mkurugenzi Mipango Bi.Mhaza Gharib katika semina ya watetezi.*

## ZLSC Yapata Afisi Mpya

**KITUO** cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kimehamia katika Afisi mpya ziliopo katika mtaa wa Migombani mkabala na *Migoz Supermarket* iliyopo katika barabara inayoelekea Uwanja wa Ndege Zanzibar.

Mkurugenzi wa ZLSC Bw. Iss-haq Ismail Shariff alisema kwamba wamehamia katika Afisi mpya April 1, 2011 kutoka afisi ya zamani iliyopo mtaa wa Kibokoni mkabala na Skuli ya Maandalizi ya Kidutani.

Alisema Afisi mpya ina vyumba vya kutosha na maktaba itakayokuwa na uwezo wa kutumiwa na zaidi ya watu 20 kwa wakati mmoja inajengwa katika afisi hiyo.

Alisema ukumbi wa maktaba pia utatumika kwa ajili ya

Inaendelea Uk. 3

## YALIYOMO

Uchomaji Moto Mabanda; Ukweli wapotoshwa Uk. 4

Ajira za Watoto ni changamoto nchini Uk. 6

Haki ya Dhamana Uk. 8

Haki za Watu wenye ulemavu Uk.12

Ripoti ya Haki za Binadamu Zanzibar 2010 yazinduliwa Uk. 18

# Bodi ya Wahariri


**Mhariri:** Prof. Chris Maina Peter

**Msaidizi Mhariri:** Iss-haq I. Shariff

**Mwenyekiti:** Harusi M. Mpatani

**Wajumbe:**
Ali Uki
Safia M. Khamis
**Msanifu**
Yussuf A. Hassan


Ifanye haki



Iwe shauku


*Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa:*
*Simu:* 0242233784
*P.O.Box:* 3360 Zanzibar
*Fax:* 0242234495
*E-mail:* zlsc@hudumazasheria.or.tz
*website:* www.hudumazasheria.or.tz


Wananchi wote mnaombwa kusoma Jarida hili la Kituo kwa madhumuni ya kujifunza zaidi na kupima maendeleo ya utendaji kazi za Kituo.
Tunakaribisha barua za maoni kutoka kwa wasomaji na michango ya makala kwa ajili ya kuelimisha umma.
Aidha wote watakaopenda kuchangia au kuleta maoni yao katika Jarida la Sheria na Haki wanatakiwa wajitambulishe kwa majina pamoja na anuani zao ili kuleta ufanisi, ukweli na uwazi katika kuendeleza Jarida hili.
Bodi ya Wahariri itakuwa na uwezo wa mwisho wa kuamua au kuhariri habari itakayochapishwa kwenye Jarida hili.Mhariri.

## Maoni ya Mhariri

# Haki na Maslahi ya Watoto Walio Katika Hali ya Kukinzana na Sheria Yazingatiwe



WANAFALSAFA mbali mbali wanaamini kwamba na madhumuni ya sheria ni kusaidia kurekebisha tabia na mwenendo wa binadamu ili jamii iweze kuishi kwa salama, amani na upendo. Ni vigumu kufikiria vipi binadamu wangeliishi bila ya kuwepo sheria. Ingekuwa vurugu tupu!

Sheria na mikataba ya kimataifa, sheria na taratibu za kitaifa kwa pamoja zimesaidia kupunguza mifarakano katika jamii. Wale wote wanaokwenda kinyume na sheria bila ya kujali hadhi au umaarufu wao katika jamii wanapambana na mkono wa sheria katika nchi zinazoheshimu utawala wa sheria.

Katika kutekeleza sheria, taasisi maalum zinazosimamia sheria (*enforcement institutions*) zimeanzishwa. Taasisi hizo ni pamoja na Polisi - sehemu ya kwanza mtuhumiwa anapofikishwa; Mahkama - sehemu ya pili ambapo maamuzi na hukumu hutolewa; na Magereza (Vyuo vya Mafunzo) wanapowekwa watuhumiwa kama mahabusu (*remandees*) au waliotiwa hatiani (*convicts*). Taasisi hizi zinaongozwa na Katiba na sheria za nchi katika utendaji wa kazi zao.

Kama tujuavyo, sheria haina macho na watu wote ni sawa mbele ya sheria. Baadhi ya wanaokinzana na sheria ni watoto (*children in conflict with the law*). Kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa wa Watoto (*United Nations Convention on the Rights of the Child - CRC*) uliopitishwa mwaka 1989 na Mkataba wa Afrika wa Haki na Maslahi ya Watoto (*African Charter on the Rights and Welfare of the Child - ACWRC*) uliopitishwa na uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Kiafrika (*Organisation of African Unity – OAU*) mwaka 1990, mtoto ni mtu mwenye chini ya miaka kumi na nane.

Lakini sheria nyingi, kama si zote, za uhalifu (*penal laws*) zinamfumbia macho mtu aliye chini ya miaka 12 mpaka 14 tu. Wote wanaoanzia miaka 14 na kuendelea sheria za uhalifu zinawabana na kuwaona kama watu wazima. Katika safu hii hatukusudii kujadili migongano ya sheria na mikataba ya kimataifa. La hasha!

Tunachokusudia kukijadili ni maslahi ya watoto (*best interests*) waliokinzana na sheria na jinsi taasisi husika, polisi, mahkama na magereza na vyuo vya mafunzo zinavyowashughulikia watoto wanaojikuta mbele ya taasisi hizi.

Tafiti zilizofanywa katika baadhi ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea zinaonyesha kwamba maslahi ya watoto hayapewi kipaumbele. Haki za watoto wanapofikishwa polisi hazizingatiwi na huchanganywa pamoja na watu wazima waliofanya makosa, jambo ambalo lazima lipigwe vita kwa nguvu zote.

Katika kusikiliza kesi hadi kufikia kutoa uamuzi baadhi ya mahkama haziangalii kwa macho ya huruma wala upendo maslahi ya mtoto kama kupata elimu, afya, kuishi na familia na haki ya kucheza. Ushahidi unapotosheleza mtoto hupewa adhabu kwa mujibu wa sheria. Hata ikiwa mkosaji ni mwanamke mwenye mtoto mdogo hupelekwa jela akiwa na mtoto wake.

Matokeo yake mtoto anaingizwa kwenye mazingira asiyostahiki na anakosa haki zake za msingi zikiwemo elimu, kuwa huru na kuchanganyika na watoto wenzake kucheza.

Kinachoumiza vichwa vyetu zaidi ni maslahi ya mtoto kutoangaliwa kwa umakini pekee (*special attention*). Watoto huchanganywa na wahalifu watu wazima katika vituo vya polisi na gerezani hawatenganishwi na watu wazima. Athari yake ni watoto kujifunza mbinu za uhalifu, kuathirika kisaikolojia na hata kuingiliwa kimwili kwa nguvu kinyume na maumbile.

Ziara iliyofanywa na maafisa mipango wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (Zanzibar Legal Services Centre - ZLSC) katika Vyuo vya Mafunzo viliopo Unguja mjini na mashamba hivi karibuni imegundua watoto kumi na wanne, wote wanaume, wamefungwa kwa makosa ya mauaji, wizi, kubaka na kupatikana na bangi kinyume na sheria.

Pamoja na makosa waliyotiwa hatiani watoto hao, hatukuridhishwa na jinsi watoto hawa waliokinzana na sheria wanavyoishi huko walikofungwa. Uongozi wa Vyuo vya Mafunzo hauzingatii Mkataba wa Haki na Maslahi ya Watoto wa Afrika (ACWRC) na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto (CRC).

Kwanza, hakuna jengo maalum (gereza) la watoto katika Zanzibar nzima. Watoto hutenganishwa na wafungwa watu wazima wakati wa usiku tu lakini kuanzia asubuhi hadi jioni wanachanganywa na wafungwa watu wazima.

Pili, watoto waliofungwa wanakosa fursa ya kupata elimu, matibabu yanayoridhisha, muda wa kufanya kazi ni mrefu, wanakosa chakula bora (*nutrition diet*), hawatengewi muda wa kucheza na mavazi yao ni kaptura hata wakati wa baridi. Kwa lugha ya jela mavazi hayo huitwa viroba.

Prof. Chris Maina Peter
Mhariri.

# Taasisi Muhimu Zakosa Viongozi Tanzania

**BAADHI** ya taasisi muhimu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimekuwa zikiendeshwa bila ya viongozi wakuu na kusababisha malalamiko ya ufuatiliaji wa haki za raia na utoaji wa maamuzi.

Kukosekana kwa viongozi wa ngazi za juu wa taasisi hizo kumesababisha watanzania kujiuliza kwamba bado kuna ukosefu wa wasomi wanaoaminika kushika nyadhifa hizo au vigezo gani vinavyozingatiwa katika kuteua viongozi?.

Taasisi zinazoendeshwa bila ya kuwa na viongozi ni Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 129 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Kukosekana kwa makamishna (kamilifu) wasiozidi watano (sasa yupo Kamishna mmoja tu) Tume hiyo haiwezi kutekeleza majukumu yake yaliyoelezwa katika Ibara ya 130 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Makamishna waliokuwepo wamemaliza muda wao.

Miongoni mwa majukumu ya Tume ni kuhamasisha nchini hifadhi ya Haki za Binadamu, kufanya shughuli za kupokea malalamiko ya uvunjwaji wa Haki za Binadamu kwa jumla na kufanya uchunguzi juu ya mambo yanayohusu uvunjwaji wa Haki za Binadamu na ukiukwaji wa misingi ya Utawala Bora.

Kwa upande wa Zanzibar, taasisi zilizokosa watendaji wakuu ni Afisi ya Mufti Zanzibar iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria ya Afisi ya Mufti Na. 9 ya 2001 ambayo miongoni mwa kazi zake ni kusimamia mambo ya waislamu na kutoa fatwa. Aliyekuwa Mufti Sheikh Harith bin Khalef alifariki dunia Agosti 26,2010.

Vile vile, nafasi ya Kadhi Mkuu wa Zanzibar ambayo imo ndani ya Sheria ya Kadhi Na. 3 ya 1985 bado ipo wazi tokea alipofariki aliyekuwa akishika wadhifa huo Sheikh Ali Khatib Mranzi.

Kutokuwepo kwa viongozi wa kushika nyadhifa hizo kunazorotesha Utawala Bora nchini .

# Maslahi ya mtoto

*Inatoka Uk. 1*

Malindi.

Miongoni mwa waliowasilisha mada ni Mhadhiri Mwandamizi wa Sheria kutoka Kitivo cha Sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Chris Maina Peter (Mikataba ya Kimataifa na Kikanda Juu ya Haki za Watoto - CRC na ACRWC), Jaji wa Mahkama Kuu Tanzania, Robert Makaramba (Mifumo ya Sheria katika Kuwalinda Watoto Tanzania) na Mhadhiri Msaidizi wa Sheria kutoka Kitivo cha Sheria Chuo Kikuu, Tunguu, Bw. Ali Uki (Udhalilishaji na Unyanyasaji wa Watoto), Bw. Khamis Yahya Hamad, Bw. Ahmed Rashid na Bw. Mohammed Jidawi juu ya Haki za Watoto. Namna ya kuendesha kesi za jinai za watoto, utafiti wa watoto wenye ulemavu ushawishi.

Akifungua semina hiyo, Mkurugenzi wa Mipango na Uendeshaji katika Wizara ya Ustawi wa Jamii Wanawake Vijana na Maendeleo ya Watoto Bi. Mhaza Gharib alisisitiza umuhimu wa haki za watoto kuheshimiwa ili kujenga taifa bora la baadae.

Bi. Mhaza aliyefungua semina hiyo kwa niaba ya Waziri Bi Zainab Omar alisema ukiukwaji wa haki za watoto unafanywa kwa visingizio visivyokuwa na misingi ya sheria.

# ZLSC yapata Afisi mpya

*Inatoka Uk. 1*

semina zinazofanywa na ZLSC ikiwemo mafunzo ya wasaidizi wa sheria (*paralegals*).

# Uchomaji Moto Mabanda: Ukweli Wapotoshwa



***Mwanasheria kutoka ZLSC, Bi. Jina Mwinyi Waziri (katikati) akizungumza na wanakijiji Pwani Mchangani kuhusiana na tukio la uchomwaji moto mabanda.***

**HIVI** karibuni tulishuhudia kitendo cha kusikitisha na kinachoashiria uvunjifu wa amani iliyopo nchini. Baadhi ya watu walichukua hatua mikononi mwao kwa kutoheshimu sheria za nchi na kuchoma mabanda ya wafanya biashara yaliyopo katika vijiji vya Pwani Mchangani na Kiwengwa katika Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Kwanza kabisa, kama wanaharakati wa Haki za Binadamu na Utawala bora tunalaani kitendo hicho kwa sababu hakikubaliki katika jamii iliyostaarabika na kinapingana na dhana ya Utawala Bora na Sheria.

Katika kadhia hii jambo moja la hatari zaidi ambalo linapaswa kulaaniwa ni udhaifu wa baadhi ya vyombo vya habari vya ndani na nje kwa kukiuka maadili ya taaluma hiyo na bila kufanya utafiti wa kutosha juu ya kadhia hiyo vilitoa taarifa potofu ya sura ya ubaguzi dhidi ya wageni (*Xenophobia*) hususan wale wanaotoka Tanzania Bara.

Kitendo cha vyombo vya habari vya kueleza picha potofu ni hatari zaidi ya kitendo cha uchomaji wa mabanda hayo. Suala la ubaguzi lilivaliwa njuga na kuhusishwa na chuki za Wazanzibari dhidi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ulioundwa April 26, 1964 na kuwaunganisha watanzania wanaotoka Tanzania Bara na waliopo Zanzibar.

Ingelikuwa sio uvumilivu na ustaarabu wa Watanzania, taarifa kama hizi zilizoandikwa na vyombo vya habari bila utafiti zingeweza kuliingiza Taifa la Tanzania katika maangamizi makubwa mithili ya maafa yaliyosababishwa na vyombo vya habari Rwanda miaka ya 1990.

Kama vyombo vya habari vingelikuwa makini na kufanya utafiti wa kutosha katika suala hilo visingeliandika habari potofu za kwamba kiini cha mabanda kuchomwa moto kwa sababu wamiliki wanatoka Tanzania Bara. Hapa tunapaswa kujiuliza, jee! kauli hizi ambazo tunaziita ni za uchochezi zilitolewa kwa nia ovu, ni bahati mbaya au ni matokeo tu?

Baada ya kutokea kwa tukio hili, Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kilifuatilia ili kupata ushahidi wa tokeo hilo. Tulifika katika eneo la tukio na kufanya mahojiano na watu mbalimbali wakiwemo wamiliki wa mabanda yaliyochomwa, wananchi wa maeneo husika, masheha na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja na tulipata picha halisi ya tukio.

Hakukuwa na hata chembe ya ushahidi ya kuhusisha kitendo cha kuchomwa moto mabanda na vitendo vya ubaguzi "*Xenophobic Practices*". Mabanda yalichomwa moto na wanakijiji wa maeneo husika waliokuwa na mivutano na wamiliki wa mabanda kwa muda mrefu. Mvutano wa pande mbili hizi ulikwishawasilishwa mbele ya vyombo vya Serikali kwa hatua za ziada.

Wanavijiji walikuwa wanadai kwamba wafanyabiashara hao walikuwa wakifanya vitendo vilivyo kinyume na maadili ya maeneo hayo na waliiomba Halmashauri ya Wilaya kuwaondosha ambayo ndio iliyoruhusu ujenzi huo.

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ilichelewa kulitolea uamuzi suala hilo, wanavijiji walipoteza stahamala na kuamua kujichukulia sheria mikononi mwao wakiamini kwamba Halmashauri haikuwa tayari kuwaondosha wafanya biashara hao kwa kuhofia kukosa mapato ya kodi.

Kitendo cha kujichukulia sheria mikononi hakikua sahihi hata kidogo na ni kinyume na Katiba zote mbili zinazoongoza nchi hii – Katiba ya Zanzibar ya 1984 na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Watu wenye asili ya Tanzania Bara wapo kila kipembe cha Zanzibar na wanafanya shughuli bila ya bughudha. Tujiulize, Jee! nao wananyanyaswa kama hawa wafanyabiashara wa Kiwengwa na Pwani Mchangani? Jibu ni hapana na hapa ndipo unapokuja ule usemi wa kiingereza "*when you are in Rome do what the Romans do*". Inadaiwa kwamba sababu kubwa ya mzozo huu ni upande mmoja kutoheshimu mila na desturi za wenyeji.

Katika utafiti wetu, tuliona watu wengi wenye asili ya Tanzania Bara wanaendelea na shughuli zao katika maeneo hayo bila ya bughudha.

Pia katika uchunguzi wetu, tulibaini kwamba baadhi ya mabanda yaliyochomwa yanamilikiwa na wazanzibari lakini ukweli huu ulifumbiwa macho kwa makusudi na vyombo vya habari. Kama waliolengwa ni watu wenye asili ya Tanzania Bara pekee , mabanda ya wazanzibari yasingelichomwa moto.

Wanaodaiwa kuchoma moto hawakuwa na ubaguzi. Walichoma kila kibanda kilichokuwepo katika maeneo yale bila ya kuangalia mmiliki ni nani. Kitu ambacho labda tunaweza kusema ni bahati tu "*Coincidence*" kwamba wengi wa wafanyabiashara waliochomewa mabanda yao moto wanatokea Tanzania Bara.

Haya pia yalithibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja Masoud Mselem Mtulia katika mahojiano alituthibitishia kwamba hakuna chembe ya ukweli wa ubaguzi "*Xenophobic Act*". Ni uhalifu wa kawaida kama uhalifu mwengine wowote ule na Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi. Wanaohusika watafikishwa mbele ya sheria.

Katika hali kama hii ni vyema vyombo vya habari vikaacha ushabiki na kufuata miiko ya taaluma badala ya kuwa sehemu ya mzozo na kujiegemeza upande mmoja na kuushambulia upande wa pili. Hali hii inafanya watu washindwe kuelewa kama vyombo hivi kweli vina maslahi na nchi hii?

# Ajira za Watoto ni Changamoto Nchini

**UTANGULIZI.**

UKIUKWAJI wa haki za watoto umekuwa ukiongezeka kwa kasi kubwa katika kila pembe ya dunia. Tafiti zinaonyesha kwamba ukiukwaji wa haki za watoto umejitokeza katika sura tofauti lakini ajira za watoto zimetia fora na zinawaathiri watoto kisaikolojia na ukuwaji wa kiujumla. Mwanasheria **SAFIA SALEH SULTAN** wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) analieleza tatizo la ajira za watoto ili watu walifahamu na kusaidiana kulipiga vita.

**MAANA YA MTOTO.**

Tafsiri ya neno mtoto imekuwa ikitofautiana kutegemea na Sheria inayofanyiwa marejeo katika nchi husika. Ibara ya 1 ya Mkataba wa Umoja wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (CRC) wa mwaka 1989 na Ibara ya 2 ya Mkataba wa Watoto wa Afrika (ACWRC) uliotayarishwa mwaka 1990 imeeleza tafsiri ya mtoto kwamba ni binadamu yoyote aliye na umri chini ya miaka 18 isipokuwa kama sheria inayotumika inatambua umri wa utu uzima kabla ya hapo.

Hata hivyo, Kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Ajira Nam. 11 ya mwaka 2005 ya Zanzibar inaeleza kwamba mtoto *"ni mtu aliye chini ya miaka 17 isipokuwa kwa shughuli za ajira katika sehemu za hatari mtoto ni kijana chini ya umri wa miaka 18".* Mswada wa Sheria ya Mtoto uliopitishwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar hivi karibuni ambao unasubiri kutiwa saini na Rais wa Zanzibar anaeleza kwamba mtoto ni yule mtu aliye chini ya miaka 18. Kifungu cha 14 (1) cha Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya 2004 mtoto asiyeweza kutenda kosa la uhalifu ni mtoto aliye chini ya miaka 12.

**MAANA YA AJIRA ZA WATOTO**

Ajira za watoto ni kuwafanyisha kazi watoto walio chini ya miaka 18 kazi ambazo hawastahiki kuzifanya kutokana na umri wao na zinaleta madhara mfano, kuwadhoofisha afya zao. Ibara ya 3 ya Mkataba wa Shirika la Kimataifa la Ajira (ILO) Nam 182 wa mwaka 1999 kuhusu mifumo mibaya ya ajira ya watoto kwamba ni kazi zozote zinazoweza kudhuru afya,usalama na maadili ya watoto.

**AJIRA ZA WATOTO NA SHERIA.**

Sheria mbali mbali zinapinga ajira za watoto. Kifungu cha 6 cha Sheria ya Ajira Nam. 11 ya 2005 inakataza ajira za watoto. Hakuna atakayeruhusiwa kumuajiri mtoto isipokuwa kwa kazi za nyumbani ambazo hazitohatarisha ustawi wa mtoto. Vile vile, Kifungu hicho kimeweka adhabu kwa mtu atakayemuajiri au kusababisha mtoto kuajiriwa kinyume na Sheria hii. Atakayetiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua shilingi laki tano (500,000/=) au kifungo kwa kipindi kisicho pungua miezi sita.

Ibara ya 32 ya Mkataba wa CRC ambao Tanzania imeridhia Disemba 02, 1990 inasema na kusisitiza *"kila mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya unyonyaji wa kiuchumi na kufanya kazi yoyote ambayo inaweza kutatiza elimu, ama kuwa na madhara kwa afya au maendeleo ya kimwili, kiakili, kiroho, kimaadili na kijamii"*



***Watoto wakiwa katika ajira***

Kushamiri ajira za watoto Zanzibar baadhi ya watu wanawafanyisha kazi ngumu watoto walio chini ya miaka 18. Mfano wa ajira hizo ni kuvua, kufanya biashara mbali mbali zikiwemo za kubanja kokoto, kufanya kazi za nyumbani (*house girl*) au kupara samaki .

Vile vile wapo watoto wanaoingizwa katika mifumo mibaya zaidi ya ajira. Tafsiri ya mifumo mibaya zaidi ya ajira za watoto inaelezwa katika Kifungu cha 7 cha sheria ya Ajira Nam. 11 ya 2005 ya Zanzibar inayojumuisha; -

a) Aina zote za matendo ya utumwa mfano uuzaji, usafirishaji, utoroshaji wa watoto, kazi za lazima na utumwa au kuajiri kwa lazima kwa ajili ya kuingia katika migogoro ya kivita.
b) Matendo ya ukahaba kwa mfano kupigwa picha za uchi au kufanya maigizo yenye picha za uchi.
c) Kuwatumilia watoto kwa kufanya kazi zisizo halali hasa ikiwemo kusafirisha madawa ya kulevya.
d) Kazi ambayo kwa mazingira yake inaweza kupelekea kupata athari ya kiafya, usalama pamoja na kuharibu maadili ya watoto.

Ili kukipa nguvu kifungu hiki sheria pia inaweka adhabu kwa atakayefanya makosa yaliyoelezwa na adhabu yake ni faini isiyopungua shilingi milioni tatu (3,000,000/=) au kifungo kisichopungua mwaka mmoja au adhabu zote mbili.

Kifungu cha 8 (i) cha Sheria hii pia kinakataza ajira kwa kijana anayesoma elimu ya lazima *(compulsory education)* mtoto ambae hayuko katika elimu ya lazima, ajira inaruhusiwa lakini kwa masharti yafuatayo:-

**i.** Asipewe kazi nzito zikiwemo za kutumia kemikali au kazi nyengine yoyote ambayo inaweza kuhatarisha afya na usalama wa mtoto.
ii. Awe anafanyiwa uchunguzi wa afya yake na daktari athibitishe kwamba mtoto huyo kulingana na umri wake anaweza kuajiriwa katika kazi hiyo.
iii. Muajiri ahakikishe kwamba mtoto aliyeajiriwa anafanya uchunguzi wa afya yake mara kwa mara mpaka atakapofikia umri wa miaka 21.

Kimsingi Sheria haimaanishi kwamba mtoto asifanye kazi yoyote. Shughuli za nyumbani ni muhimu kushiriki kwasababu kazi ni sehemu ya ukuaji wa binadamu. Ajira inayokatazwa kwa watoto ni ile yenye uwezekano wa kumnyima mtoto haki ya elimu, kiukuaji katika maeneo ya saikolojia, kimwili, kihisia, kiakili na kimaendeleo. Ajira zinazohusisha kazi nzito na mazingira magumu ya afya na mengineyo kulingana na umri wao. Hata hivyo, malipo wanayopewa watoto ni duni yasiyolingana na kazi wanazofanya.

**MADHARA YATOKANAYO NA AJIRA ZA WATOTO.**

Ajira za watoto ni kikwazo katika ukuaji wa kimwili, kimaono na kijamii. Watoto wanaoathirika kimwili, kisaikolojia, wanakosa haki zao za msingi na mambo mengine baadhi ni haya yafuatayo;

1. Kukosa elimu.
2. Watoto wanaathirika sana kisaikolojia na kiafya.
3. Huchangia mmongo'nyoko wa maadili na utamaduni.
4. Ongezeko la mimba za utotoni.
5. Ongezeko la vifo vya watoto au ulemavu; kwa mfano wanaoajiriwa migodini na uchumaji wa karafuu.

**CHANGAMOTO**

Baadhi ya changamoto zinazowafika watoto katika jamii ni hizi zifuatazo;

1. Mipango endelevu ya uondoaji ajira za watoto katika hali ya umasikini.
2. Ukimwi unaoacha mayatima.
3. Utunzaji wa watoto
4. Ukosefu wa elimu kuhusu haki za watoto.

**SULUHISHO**

Baadhi ya ufumbuzi wa changamoto za matatizo ya watoto ni;

1. Mzazi/ mlezi ahakikishe anawatunza na kuwapatia huduma zote muhimu watoto.
2. Wazazi waelewe elimu ni silaha ya kuwalinda watoto dhidi ya dhulma zinazowakabili.
3. Serikali ifuatilie ustawi wa watoto na kuwadhibiti wanaowatumikisha watoto kwa maslahi yao binafsi.
4. Jamii itambue tatizo la ajira za watoto na kupambana nalo.

**HITIMISHO**

Mtoto ana haki ya kulindwa, kuthaminiwa na kupewa haki zote ili kumjenga kimawazo, kifikra na kiakili. Watoto ni hazina na wanayo nafasi ya kutoa mchango kwa maendeleo ya taifa na dunia. Ni jukumu la kila mtu katika jamii kuimarisha maslahi ya watoto (*best interests of the child).*

# Haki za Binadamu Magerezani

**UTANGULIZI**

**MAAFISA** wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) walifanya ziara katika Vyuo vya Mafunzo Unguja hivi karibuni kwa madhumuni ya kufanya tathmini ya Haki za Binadamu zinavyotekelezwa katika Vyuo vya Mafunzo. Vyuo vya Mafunzo vilivyotembelewa ni Kiinua Miguu, Kinu Moshi, Langoni, Ubago, Hanyegwa-Mchana na Bumbwini Mafufuni. Mwanasheria **MAKAME MAHMOUD KHAMIS** anatoa muhtasari wa tathmini ya Haki za Binadamu magerezani, Unguja.

**HISTORIA YA JESHI LA CHUO CHA MAFUNZO**

Sheria ya kwanza iliyoanzisha Jeshi la Chuo cha Mafunzo Zanzibar ni ya mwaka 1933 iliyotambulika kuwa ni Sheria ya Magereza, Sura ya 51. Sheria hii ilifutwa mwaka 1972 kwa Sheria Nam. 2 ya 1972. Sheria hizi zilipitwa na wakati na zilifutwa na Sheria Nam. 1 ya 1980 ya Chuo cha Mafunzo inatumika sasa. Jeshi la Chuo Cha Mafunzo limeanzishwa chini ya Kifungu cha 121 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Jeshi hilo ni sehemu ya Idara Maalumu za Vikosi vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kifungu hicho kinaeleza kwamba *"kutakuwa na Idara Maalumu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo kazi zake na shughuli zake zitakuwa kama zitakavyoainishwa katika sheria zinazohusika."* Sheria iliyoanzisha Chuo cha Mafunzo ni Sheria Nam 1 ya 1980 na marekebisho yake yaliyofanywa chini ya Sheria Nam.3 ya 2007.

**KANUNI ZA KIMATAIFA KUHUSU HAKI ZA WATU WALIOPO MAGEREZANI**

Kanuni zilizowekwa na Jumuiya ya Kimataifa zinazopaswa kuheshimiwa na nchi wanachama zinapotunga sheria zinazohusu magereza ni hizi zifuatazo:

[a] Kanuni za Msingi za Kimataifa kuwashughulikia wafungwa magerezani za mwaka 1990.

[b] Kanuni za Kiwango cha Chini za Kimataifa katika kuwashughulikia wafungwa magerezani 1957

[c] Kanuni za Kushughulikia Watu Walioko Kizuizini [wafungwa] ya mwaka 1990.

[d] Kanuni za Umoja wa Mataifa juu ya kinga kwa Watoto Waliozuiliwa uhuru wao kuhakikishiwa haki kwa kinga dhidi ya adhabu ya kifo ya mwaka 1990

[e] Kanuni za Umoja wa Mataifa kuhusu Viwango vya Chini juu ya Haki za Watoto waliozuiliwa Uhuru wao ya mwaka 1985.

[f] Haki za Watoto katika Mkataba wa Kimataifa wa

Inaendelea Uk. 5



*Maafisa wa Magereza Zanzibar wakiwa katika semina ya watoto.*

# Haki za Binadamu Magerezani

*Inatoka Uk. 4*

mwaka 1989 unakwenda sambamba na Mkataba wa Watoto wa Afrika 1999

[g]Kanuni zinazotumika kuwashughulikia rumade magerezani za mwaka 1957 na mwaka 1977

## MAMBO YA MSINGI YANAYOPASWA KUANGALIWA KWA WATU WALIOPO MAGEREZANI

[1] Makaazi ya wanafunzi [wafungwa]

[2] Vyoo

[3] Mlundikano wa rumande.

[4] Lishe ya wafungwa

## HALI HALISI YA VYUO VYA MAFUNZO ZANZIBAR

Hali halisi ya wafungwa katika Vyuo vya Mafunzo Zanzibar kulingana na vigezo vifuatavyo ni;

## MAKAAZI YA WANAFUNZI

Asilimia kubwa ya majengo wanayoishi wafungwa ni ya zamani na yapo chini ya kiwango kilichoelezwa katika kilichoelezwa katika Kanuni za Kimataifa. Wafungwa na mahabusu wanaishi pamoja. Watoto wanaishi pamoja na wafungwa watu wazima isipokuwa wakati wa usiku wanatenganishwa. Vyoo vinavyotumiwa na wafungwa ni mitondoo (wanakwenda haja katika ndoo).

## MALAZI NA HEWA SAFI

Malazi ya wafungwa na mahabusu hayaridhishi. Msongamano mkubwa upo katika vyumba vya kulala. Aidha, hewa safi inayopatikana



***Baadhi ya maafisa wa Magereza wakisiliza maelezo kutoka kwa Maafisa Mipango wa ZLSC.***

kupitia madirisha madogo haitoshelezi.

## CHAKULA

Wafungwa hawapati mlo wa kutosha na chakula hakizingatii sifa ya chakula bora (*nutrition food).*

## MRUNDIKANO WA RUMANDE

Idadi ya watu waliopo rumande ni kubwa mno. Hali hiyo inachangiwa na masharti magumu yanayotolewa na Mahkama kwa ajili ya kuomba dhamana au kunyimwa dhamana.

## MAPENDEKEZO YAFUATAYO YAZINGATIWE ILI KUBORESHA HALI YA MAGEREZA

**(1)**Haki za Binadamu kwa wafungwa ziheshimiwe.

**(2)**Mahkama isiwe kikwazo cha kutoa dhamana

**(3)**Wafungwa waruhusiwe kukatana na familia zao, wanasheria, daktari, viongozi wa dini zao na wageni wengine.

**(4)**Maazimio ya Kimataifa na Kikanda kuhusu haki za wafungwa yaheshimiwe.

**(5)** Mgao wa fedha za bajeti ya Serikali uongezwe kwa Idara hii iongezwe ili kuiwezesha taasisi hii kutekeleza malengo yake.

**(6)**Uongozi wa Vyuo vya Mafunzo ubuni miradi ya kuzalisha mali ili ipate fedha badala ya kutegemea fedha kutoka Serikalini.

## HITIMISHO

Haki za Binadamu katika Vyuo vya Mafunzo Zanzibar ipo chini ya kiwango. Mabadiliko lazima yafanywe ili kuboresha Haki za Binadamu. Taasisi za Serikali na Kiraia kutoka ndani na nje ya nchi zisaidie kuboresha Haki za Binadamu katika Vyuo vya Mafunzo Zanzibar.

# Haki ya Dhamana

**UTANGULIZI**

**DHAMANA** ni haki ya kikatiba anayostahiki kupewa mshtakiwa au washtakiwa wanaokabiliana na kosa au makosa ya jinai. Mahkama, taasisi huru inayotathmini uzito wa kesi na kuamua (*discretion*) aina ya masharti ya dhamana ili kuhakikisha mshtakiwa anafika Mahkamani siku na wakati anaotakiwa kuwepo bila ya kukosa. Utoaji wa dhamana umekuwa mgumu ama kwasababu ya masharti magumu yanayowekwa na Mahkama kufuatana na uzito wa kesi na jinsi Mahkama inavyoshawishika kama mshtakiwa atafika Mahkamani atakapohitajika. Lakini, utoaji wa dhamana unatawaliwa na vigezo vinavyokiuka au vinavyoashiria kukiuka Haki za Binadamu. Mwanasheria **LATIFA SALEH, anaelezea** dhana nzima ya dhamana.



*Chumba cha mahabusu.*

**MAANA YA DHAMANA**

Dhamana ni njia ya kukabidhisha Mahkamani mali au fedha taslimu au kwa njia ya maandishi kwa lengo la kutaka mshtakiwa au washtakiwa waliopo kizuizini waachiliwe kwa muda kwa kuamini kwamba mshtakiwa huyo atafika mahakamani siku na wakati atakaotakiwa.

**UMUHIMU WA DHAMANA**

Umuhimu wa dhamana ni kuhakikisha mshtakiwa au washtakiwa wanafika Mahkamani siku na wakati watakaotakiwa bila ya kukosa. Kitendo cha kukabidhisha mali au fedha Mahkamani kabla ya kutolewa dhamana ni kuifanya Mahkama iamini kwamba mdhamini atahakikisha kwamba mshtakiwa hatoroki na anafika Mahkamani kama inavyotakiwa. Mahkama inaweza kukataa kutoa dhamana kutokana na mazingira ya kesi hususan ikiwa zipo dalili kwamba mshtakiwa hatofika Mahkamani.

**MAKOSA YASIYOTOLEWA DHAMANA**

Baadhi ya nchi zimeweka baadhi ya makosa ambayo hayatolewi dhamana. Kwa mfano, Kifungu cha 150 (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai Na. 7 ya 2004 imesema kwamba makosa ya mauaji au uhaini au wizi wa kutumia nguvu (*armed robbery*) au kupatikana na silaha za moto au madawa ya kulevya, hayatolewi dhamana.

**PESA AU MALI ILIYOWEKWA DHAMANA**

Fedha au mali iliyowekwa dhamana inarudishwa kwa mhusika mwisho wa kesi bila ya kujali mshtakiwa ametiwa au hakutiwa hatiani ameadhibiwa au hakuadhibiwa au kinaweza kutaifishwa ikiwa mshtakiwa atashindwa kufika mahkamani.

**AINA ZA DHAMANA**

i Dhamana ya polisi kabla ya kufunguliwa mashtaka:

Hii ni aina ya dhamana anayopewa mtuhumiwa katika kituo cha polisi kabla ya kufikishwa Mahkamani. Mtuhumiwa atalazimika kurejea polisi atakapohitajika.

ii Dhamana ya Mahakama:

Mshtakiwa ana haki ya kupata dhamana ilimradi anatimiza masharti ya dhamana wakati kesi inaendelea. Mahkama ina uwezo wa kumnyima muomba dhamana ikiwa zipo sababu za msingi zinazoonesha kuwa kumpatia mtuhumiwa dhamana kutapelekea haki kutofikiwa. Katika kesi ya ***TITO DOGLAS LYMO V. R*** (1979) LRT no 55, Jaji Mwesiumo, katika kesi hii iliamuliwa kwamba dhamana ni haki ya mshtakiwa na sio upendeleo, na hivyo Mahakama haitakiwi kumnyima labda kuwe na sababu za msingi zinazoonyesha kuwa kumpatia mshtakiwa dhamana kutapelekea haki kutokufikiwa na mahakama.

**Zipo aina mbili za Dhamana za Mahkama:**

**i.** Dhamana kabla ya kesi kumaliza kusikilizwa.

Hii ni aina ya dhamana ambapo mshtakiwa anaweza kuiomba Mahkama kumuachia mpaka kesi itakapomaliza kusikilizwa. Mahakama itaweka masharti na yakitimizwa dhamana itatolewa. Kwa mujibu wa sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai Na. 7 ya 2004 aina hii ya dhamana ni haki ya mshtakiwa na hatakiwi kunyimwa. Katika kesi ya ***DAUDI s/o PETE V.*** **THE UNITED REPUBLIC.** ***High court*** of Mwanza, Mislaneous Criminal case no. 80 of 1989. Mshtakiwa wa kosa la wizi wa kutumia nguvu alinyimwa dhamana na Mahkama ya Wilaya na akaamua kukata rufaa Mahkama Kuu na kuamuliwa kwamba dhamana ni haki ya mshtakiwa na sio kitu cha upendeleo, kumnyima dhamana ni kupingana na dhana ya kuwa kila mtu hana kosa hadi itakapothibitishwa na Mahkama kuwa ni mkosa.

Aina hii ya dhamana huombwa kabla ya mshtakiwa kutiwa hatiani, hivyo ni haki yake na haipaswi kumnyima bila ya kuwa na sababu za msingi.

**ii.** Dhamana baada ya kumalizika kesi na kabla ya rufaa.

Hii ni aina ya dhamana inayoombwa na mtu aliyetiwa hatiani na kuhukumiwa kifungo. Inaombwa baada ya kumalizika kesi na anayetarajia kukata rufaa kutoridhika kutiwa hatiani au adhabu au yote mawili. Aina hii ya dhamana sio haki ya mtuhumiwa kwasababu tayari Mahkama imeshamtia hatiani. Mahkama inaweza kutoa dhamana hii kama tunuku (*privilege*) tu pale Mahkama itakapoona inafaa na kwa kuzingatia mazingira ya kesi.

Kwa msingi huu, dhamana ni haki ya mshtakiwa kabla ya kutiwa hatiani kwa kosa analoshtakiwa. Kifungu cha 12 (6) (b) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 inaeleza kwamba *"mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai hatatendewa kama mtu mwenye kosa hilo mpaka itakapothibitika kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo."*

**MAMBO YA KUZINGATIA KABLA YA KUTOA DHAMANA**

Mahakama kabla ya kutoa dhamana inalazimika kuangalia mambo yafuatayo;

i. Uhalisia na uzito wa kosa analotuhumiwa muomba dhamana kulitenda, na makosa yanayoweza kutokea ikiwa atapewa dhamana na namna ya kuyatatua pindipo

*Inaendelea Uk. 9*

# Haki ya Dhamana

*Inatoka Uk. 8*

yakitokea.
ii. Tabia za mtuhumiwa tangu awekwe kizuizini, matukio yanayojitokeza yanayohusiana na kosa lile, pamoja na matendo ya jamii iliyomzunguka mtuhumiwa kwa wakati ule.
iii. Kumbukumbu zilizopita za dhamana kwa mtuhumiwa.
iv. Uzito wa ushahidi.

### KUKATALIWA DHAMANA

Mahakama inaweza kumnyima mshtakiwa dhamana licha ya kuwa hii ni haki yake kwa sababu zifuatazo;

1) Usalama wa mtuhumiwa/mshtakiwa: Mahakama inaweza kukataa dhamana ikiwa itakuwa na ushahidi wa kujitosheleza kuonyesha kwamba kumpatia dhamana mtuhumiwa kurudi katika jamii kunaweza kuhatarisha maisha ya mtuhumiwa. Mahakama huangalia tabia ya jamii dhidi ya mtuhumiwa au familia ya muathirika wa kosa lile.
2) Ikiwa Mahkama inaamini kwamba, mtuhumiwa atatoroka (hatorudi tena mahakamani) au atatenda kosa jengine linalohusiana na kosa lililotendwa au atawakera au kuwatishia mashahidi wa kesi ile.
3) Ikiwa Mahkama inaamini kwamba kumtoa mtuhumiwa kutasababisha kukosekana kwa habari muhimu zinazohusiana na kesi.
4) Ikiwa mtuhumiwa anatumikia kifungo cha kesi nyengine.
5) Ikiwa mshtakiwa ameshawahi kukimbia baada ya kupewa dhamana kwa kesi hiyo hiyo anayoiombea dhamana.
6) Ikiwa mtuhumiwa ameshtakiwa kwa kosa ambalo halitakiwi kupewa dhamana kwa mujibu wa sheria.

### MASHARTI YA DHAMANA

Baadhi ya Mahkama au polisi huweka masharti maalum kwa ajili ya dhamana ili kumuwezesha muomba dhamana afike Mahkamani atakapohitajika. Masharti yanategemea sheria za nchi husika au mazingira ya kesi ilivyo. Mfano wa masharti ni haya yafuatayo;

- Kumtaka mshtakiwa akae katika eneo maalum bila ya kuhama.
- Kuripoti katika kituo maalum cha polisi kila baada ya muda.
- Kutokutoka nje ya eneo maalum.
- Kusalimisha pasi (*passport*) ya kusafiria
- Kutoa kidhamini cha pesa kama itakavyoamua mahakama.
- Kuleta mdhamini (*surety bond*), ambaye atakuwa ni mtu anayemjua mshtakiwa/mtuhumiwa, na ambaye ataahidi kutoa kiasi maalum cha fedha au waraka wa nyumba au shamba lenye thamani ya kiwango kinachotakiwa kwa ajili ya dhamana. Iwapo mshtakiwa au mtuhumiwa atashindwa kufika Mahkamani kwa muda uliopangwa. Pia mdhamini anaweza, baada ya kufuatwa utaratibu ikiwemo kupewa muda zaidi wa kumtafuta mshtakiwa, kufungwa iwapo atashindwa kumfikisha Mahkamani mshtakiwa na atashindwa kulipa pesa alizoahidi.

### KUVUNJA DHAMANA

Mshtakiwa aliyeachiwa huru kwa dhamana, atatakiwa kufika Mahkamni kila atakapohitajiwa kwa ajili ya kesi inayomhusu. Kutohudhuria Mahkamani bila ya sababu zinazokubalika itakuwa ni kosa na Mahkama inaweza kuifuta dhamana na inaweza kupelekea Mahkama kutompa mshtakiwa dhamana nyengine iwapo ataiomba kwa kutoaminika.

### UTARATIBU WA KUTOA DHAMANA MAHKAMANI

Mshtakiwa anatakiwa aombe dhamana Mahkamani siku ya mwanzo kesi inapoanza kutajwa. Hakimu au jaji anatakiwa kuuliza upande wa pili wa kesi (Mwendesha Mashtaka) kutoa maoni iwapo kuna pingamizi dhidi ya maombi hayo. Ikiwa hakuna pingamizi Mahkama itatoa masharti ya dhamana kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vya kesi hiyo.

Iwapo Mahkama itamnyima dhamana mshtakiwa, haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi au masharti yaliyowekwa ipo kwa mshtakiwa. Rufaa itafunguliwa katika Mahkama ya juu ya ile iliyosikiliza kesi iliyoombewa dhamana.

Vile vile Kifungu cha 150(4) cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai, kinaipa mamlaka Mahkama Kuu kuweza kuipa maelekezo Mahakama yeyote iliyo katika ngazi ya chini kumpatia mshtakiwa dhamana au kuamrisha masharti ya dhamana yaliyowekwa na Mahkama ya chini au afisa wa polisi kupunguzwa.

### HALI HALISI ILIVYO KWA SASA

Haki ya kupata dhamana kwa mshtakiwa imekuwa ni kikwazo. Masharti magumu huwekwa kwa makusudi yasiweze kutimizwa ili mshtakiwa aendelee kubakia rumande kwa muda mrefu. Kifungu cha 150 (3) cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai kinaipa mamlaka Mahkama kuamua kiasi cha fedha kama ni dhamana lakini kiwango hicho kisiwe kikubwa sana. Ongezeko la mahabusu bila ya sababu ya msingi kunaiongezea mzigo wa gharama Serikali. Idadi ya rumande iliyopo mahabusu katika Chuo cha Mafunzo, Kilimani, ni zaidi ya 200. Mahabusu wengi wanashtakiwa makosa ambayo sheria haijakataa kutolewa dhamana.

Kifungu cha 151(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai kinaeleza kwamba makosa yasiyotolewa dhamana, muda wa kuanza kusikilizwa kesi ni miezi tisa baada ya tukio. Zaidi ya hapo mtuhumiwa anatakiwa apewe dhamana au Mahkama itoe sababu za msingi za maandishi kwa nini dhamana isitolewe.

Ikiwa kosa ni la kupewa dhamana na miezi minne ikimalizika ushahidi haujatimia, kesi ifutwe. Upungufu wa sheria hii haijamlazimisha hakimu kuifuta kesi bali imempa hiari.

### HITIMISHO

Dhamana ni haki ya mshtakiwa iliyowekwa kisheria. Mahakimu na majaji wanatakiwa watumie Mamlaka waliyopewa kutoa dhamana kulingana na vigezo vya kisheria.



*Mahabusu akiingizwa rumande baada ya kukosa dhamana.*



*Maafisa Mipango wa ZLSC wakifahamishwa mradi wa ufugaji wa samaki katika kambi ya Bum*



*Ripoti ya Haki za Binadamu 2010 ikizinduliwa Dar es Salaam.*




*Uzinduzi wa Agenda za watoto Zanzibar.*



*Baadhi ya waliochomewa moto mabanda*
*msaada.*



bwini.



Mwenyekiti wa ZLSC Prof. Chris Peter akizungumza katika uzinduzi wa Ripoti ya Haki za Binadamu ya 2010 Zanzibar.



Baadhi ya Majaji, Mahakimu na Makadhi waliohudhuria semina ya siku mbili ya Haki za Watoto Zanzibar



a Pwani Mchangani wakipewa



Baadhi ya wataalamu wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) wakiwa katika picha pamoja na baadhi ya maafisa wa magereza walipotembelea magereza ya Unguja.

# Haki za watu wenye ulemavu

**UTANGULIZI**:

**KATIKA** kila jamii wapo baadhi ya watu walemavu wa aina moja au nyengine ambao wanahitaji msaada ili kutimiza mahitaji yao. Ulemavu unasababishwa na mambo tofauti. Wapo watu wanaozaliwa na ulemavu, wapo watu waliopata maradhi na kuugua kwa muda mrefu na hatimaye kupata ulemavu na wapo waliopata ajali za aina tofauti ikiwemo vita, ajali za gari, ndege na hata kuanguka kutoka juu ya miti. Waswahili wanasema watu wote ni walemavu watarajiwa. Kwa msingi huu haki za watu wenye ulemavu lazima ziheshimiwe na nchi zinahitajika kutenga sheria za haki za watu walemavu, Mwandishi **SITI HABIB MOHAMMED** wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) anaelezea kuhusu haki za watu wenye ulemavu.

### MAANA YA ULEMAVU

Ulemavu ni hali ya kuwa na viungo au kiungo cha mwili chenye hitilafu au ni hali ya kulemaa kwa viungo.

### AINA ZA ULEMAVU

Zipo aina nyingi za ulemavu. Baadhi ya aina za ulemavu ni hizi zifuatazo;

Ulemavu wa viungo: Ni ule ambao unaowakabili watu wasioona, wasioweza kusikia na wenye hitilafu ya viungo kama miguu au mikono na akili. Ulemavu wa aina hii unaweza kuupata tangu kuzaliwa kwako au baada ya kuzaliwa

Ulemavu wa ngozi (*Albino*): Mtu mwenye ulemavu wa ngozi. Mara nyingi ulemavu huu unampata mtu tokea kuzaliwa kwake.

Ulemavu wa mtindio wa ubongo: Huu ni ulemavu ambapo mtu anazaliwa akiwa na kichwa kikubwa, zaidi ya kichwa cha kawaida au pia ulemavu huu unawafanya watu wa aina hii kufanana sura hata kama wanatofautiana rangi za mwili.



*Mtoto mwenye ulemavu akiwa amepumzika katika baiskeli.*

### SABABU NA ATHARI ZA ULEMAVU

Ulemavu unaweza kupatikana kutokana na sababu nyingi. Miongoni mwa sababu hizo ni:

i) Unaweza kuupata kwa kuzaliwa.
ii) Unaweza kuupata kwa kupatwa na ajali
iii) Unaweza kuupata kwa ugonjwa
iv) Unaweza kuupata kwa kutumia lishe duni.

Kuna watu wanaozaliwa na ulemavu na wengine huzaliwa wakiwa hawana ulemavu lakini wakapata ulemavu katika maisha yao. Ulemavu sio kasoro na watu wote wapo sawa mbele ya macho ya sheria.

### UKATILI DHIDI YA WATOTO WALEMAVU KATIKA NYUMBA ZA KULELEA WATOTO

Watoto wenye ulemavu walio katika rika mbalimbali hufanyiwa ukatili na walezi wao katika nyumba za kulelea watoto. Ukatili huu ni wa kimwili, hasa matendo ya ngono, kihisia na kimaneno. Mara nyingi watoto hawa husahaulika na kutengwa kwa kiasi kikubwa. Pia watoto walemavu huwekwa katika mazingira ya kiutumwa au kama wafungwa. Wanakaa peke yao, wanatengwa na wanakosa upendo kutoka kwa walezi na watoto wenzao. Hivyo watoto wenye ulemavu hujisikia hunyanyasika na kudhalilika. Jamii inatakiwa iweke mazingira mazuri katika nyumba wanazoishi watu wenye ulemavu.

### ULEMAVU NA JAMII YA KIMATAIFA

Jamii ya Kitaifa na Kimataifa kwa pamoja zinatambua hali ya watu wenye ulemavu, mapungufu yao na matatizo wanayokabiliana nayo. Kwa msingi huu, jamii ya Kimataifa Umoja wa Mataifa (United Nations) na taasisi zake umepitisha maazimio mengi yanayolenga katika kuwasaidia walemavu.

Miongoni mwa maazimisho hayo ni:

- Mwaka wa Kimataifa wa Walemavu – *1981* (International Year of Disabled Persons (IYDP) (1981)
- Miaka Kumi ya Umoja wa Mataifa kwa Walemavu 1983–1992 (United Nations Decade of Disabled 1983 – 1992)
- African Decade of Disabled Persons (2000-2009)
- World Programme of Action Concerning Disability Persons (3rd December 1982)

Maazimio haya yote yanalenga na kusisitiza kuhusu kulinda na kuheshimu hadhi ya watu wenye ulemavu na kukataza aina yoyote ile ya ubaguzi kwa watu wenye ulemavu. Pia maazimio yanazitaka nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa kuweka na kuanzisha mikakati ambayo itasaidia kufanya watu wenye

*Inaendelea Uk. 13*

# Haki za watu wenye ulemavu

*Inatoka Uk. 12*

ulemavu kujitegemea.

### HAKI ZA WATU WENYE ULEMAVU

Watu wenye ulemavu wanatakiwa kupewa haki sawa kama binadamu wengine. Haki hizo pia zimeelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya 1984 na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Haki za watu wenye ulemavu pia zimeelezewa katika sheria na maazimio mengine kama Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa )Nam. 9 ya Mwaka 2006, Zanzibar. Haki wanazostahili watu wenye ulemavu hizi zifuatazo;

i) Usawa mbele ya sheria: Watu wote ni sawa mbele ya sheria kama ilivyoelezewa katika Kifungu cha 12 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kwamba "*watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.*"

ii) Haki ya kuwa sawa kama binadamu wengine: Kifungu cha 11 (2) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinaeleza kwamba *"kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake".*

iii) Haki ya kuwa hai: Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake. Kifungu cha 13 (2) Katiba ya Zanzibar ya 1984.

iv) Haki ya kuwa huru: Kifungu cha 14(1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kinaeleza kwamba *"kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru".*

v) Haki ya kupewa uangalifu na matunzo bora: Mtu yoyote mwenye mtoto aliye na ulemavu ana wajibu wa kumpatia uangalifu na matunzo bora kulingana na mahitaji yake kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (1) cha Sheria Nam 9 ya 2006, Zanzibar. Sheria ya Watu Wenye Ulemavu (Haki na Fursa).

vi) Haki ya kupatiwa elimu: watu wenye ulemavu wana haki ya kupata elimu bila ya kujali kuwa kwake mlemavu. Kifungu cha 9 cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Nam. 9 ya 2006 ya Zanzibar *"kwamba watu wenye ulemavu wanayo haki ya kupatiwa elimu kama binadamu wengine".*

vii) Uhuru wa kwenda anakotaka: Pia mtu mwenye ulemavu anayohaki ya kuwa huru na kwenda atakako kama binadamu wengine na sio kuwekwa kizuizini ili kumzuilia haki yake kama wanavyofanya baadhi ya watu katika jamii.

viii) Haki ya kupata ajira: Kifungu cha 7 cha Sheria ya Watu Wenye Ulemavu imeeleza kwamba "*ukiachana na sheria nyengine zinazohusiana na ajira hakuna mtu yoyote atakayemkana au kumkataa mtu mwenye ulemavu kutokana tu na kuwa na kiwango kidogo katika ajira hiyo".* Pia Kifungu cha 22 (1) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 kimeeleza kwamba *"kazi pekee ndiyo huzaa utajiri wa mali katika jamii, ndio chimbuko la ustawi wa wananchi na kipimo cha utu, kila mtu anao wajibu wa: (a) kushiriki kwa kujituma na kwa uaminifu katika kazi halali na uzalishaji mali".* Hivyo ni wajibu wakila waajiri kuwapatia walemavu nafasi za ajira kwenye maidara yao kama wanavyowapatia watu wengine.

Kwa muhtasari hizo ni miongoni mwa haki ambazo mlemavu anastahili kupatiwa kama wanavyopatiwa binadamu wengine kwasababu wanastahiki.

### WATU WENYE ULEMAVU NA AJIRA

Kuna tafauti kubwa sana kuhusu ajira ya walemavu kinadharia na vitendo. Hali halisi inatofautiana na matendo ya baadhi ya watu katika jamii.

Kifungu cha 7 cha Sheria Nam. 9 ya 2006 ya *Sheria ya Zanzibar ya Watu wenye Ulemavu kwamba "hapana mtu atakayekataa kumuajiri mtu au mtu mwenye ulemamavu mwenye sifa za kiwango cha chini za kuajiriwa"* Sheria hii inahusu sekta za umma na binafsi.

### KUFUKUZWA KAZI KWA WATU WENYE ULEMAVU

Kifungu cha 16 cha Sheria ya Ajira Nam 11 ya 2005 kinaeleza kwamba *"kukitokea ufukuzwaji wa wafanyakazi katika taasisi fulani basi walemavu wasihusishwe kabisa katika zoezi hilo".* Ni kosa la jinai kumnyima kazi au kumpunguza kazini mtu mwenye ulemavu mwenye sifa kwa sababu tu ya ulemavu wake.

### ADHABU KWA MWENYE KUMFUKUZA KAZI MTU MWENYE ULEMAVU

Kifungu cha 22 kinasema ni kosa kumbagua mtu mwenye ulemavu au kifungo kisichozidi miezi 5 au adhabu zote mbili kwa pamoja.

### CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WATU WENYE ULEMAVU

Katika jamii zetu kuna watu wenye ulemavu wa aina tofauti na wanakumbana na changamoto mbali mbali katika mfumo wao mzima wa maisha. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo;

- Kutelekezwa.
- Kutopatiwa haki ya elimu.
- Kunyimwa nafasi za ajira.
- Kubakwa na kupatiwa mimba za utotoni.
- Kutokupewa haki ya kwenda wanakokutaka:

### HITIMISHO

Serikali ihakikishe kwamba kila anayefungua kituo cha kulea watoto ni lazima awe na watu wenye utaalamu wa kulea watoto wenye ulemavu kinyume chake kituo hicho kisipewe ruhusa ya kulea watoto wenye ulemavu ili kuepusha ukatili. Aidha, Serikali itengeneze miongozo ya Vituo vya Kulea Watoto na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara na itakapobainika Kituo kinakiuka Sheria na Miongozo kifungiwe.

Vile vile, jamii ishirikiane na kuwalea watu wenye ulemavu katika mazingira mazuri na yaliyo bora ili kuwaepushia misukosuko wanayokumbana nayo. Tuwathamini, tuwaenzi, tuwaheshimu na tuwajali walemavu kwasababu ni binadamu sawa na binadamu wengine.

# Ijue Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja

**UTANGULIZI**

**TATIZO** la watoto wa mzazi mmoja linaendelea kujichomoza kwa kasi kubwa Zanzibar na kusababisha ukosefu wa malezi na matunzo sahihi kwa watoto. Mwanasheria wa ZLSC **KHALFAN AMOUR** anatizama athari ya tatizo na kuangalia nafasi ya kuwalinda wari na watoto wa mzazimmoja Nam 4 ya 2005 katika kukubaliana na tatizo hilo muhimu.

Kifungu cha 2 cha Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa MzaziMmoja Nam. 4 hii kinatoa baadhi ya tafsiri ya maneno yaliyotumika katika Sheria hii ni mwari mwanamke mwenye umri baina ya miaka 18 na 21 na ambaye hajawahi kuolewa wala hajawahi kuzaa.

**MAANA YA MTOTO WA MZAZI MMOJA**

Kifungu cha Sheria ya hii na mtoto wa Mzazimmoja ni mtoto ambaye amezaliwa nje ya ndoa.

**MWARI ALIYEPATA UJAUZITO**

Mwari anaweza kupata ujauzito kwa ridhaa au bila ya ridhaa yake. Kifungu cha 3 (1) cha Sheria hii inaeleza kwamba mwari atakayepata ujauzito kwa hiari yake atakuwa ametenda kosa.

Mwari hatohesabiwa amepata uja uzito kwa hiari ikiwa uja zito ameupata kwa kubakwa bila ya kuangalia ubakaji umetolewa taarifa katika mamlaka husika au ikiwa uja uzito umepatikana kutokana na ushawishi usiostahiki au kwa kitendo ambacho kimemnyima mwari kuwa na ridhaa ya kufanya tendo la ndoa baina ya watu ambao hawajaoana kisheria na kitendo hicho kikamsababishia uja uzito.

Kifungu cha 3 (6) cha Sheria hii Nam. 4 ya 2005 kinasema kwamba mwari atakayetiwa hatiani kwa kupata ujauzito kwa hiari atalazimika kuitumikia jamii kwa kipindi cha miezi sita kipindi ambacho kitaanza baada ya kujifungua.

**MTU ALIYEMPA MWARI UJA UZITO**

Kifungu cha 3 (3) cha Sheria hii kinasema kwamba mtu atakayetiwa hatiani kwa kumpa uja uzito mwari atahukumiwa kifungo kisichopungua miaka mitatu na kisichozidi miaka mitano.

Vile vile, Kifungu cha 3 (4) cha Sheria hii kimesema mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa la kumpa ujauzito mwari, ataamriwa kutoa matunzo kwa mtoto aliyezaliwa. Lakini ikiwa mtu aliyetiwa hatiani ni mwanafunzi mwenye umri usiozidi miaka 18, atatakiwa kuitumikia jamii kwa muda utakaoamuliwa na Mahkama.

Kifungu cha 4 (5) cha Sheria hii kinaeleza kwamba mwanafunzi mwenye umri wa chini ya miaka 18 atakayetiwa hatiani kwa kumpa uja uzito mwari atasimamishwa masomo lakini anaweza kurejeshwa skuli mwaka wa masomo unaofuata baada ya kumaliza kuitumikia jamii. Lakini Mamlaka ya Elimu inaweza kumrudisha katika muda wowote itakayoona unafaa. Muda huo usizidi miaka miwili ya masomo.

**ULINZI JUU YA HAKI YA KUPATA ELIMU**

Kifungu cha 4 (1 - 5) cha Sheria hii kinaeleza kwamba mtoto wa kike atakayepata uja uzito akiwa yupo skuli atasimamishwa masomo. Lakini mtoto huyo anaweza kurejea skuli mwaka unaofuata baada ya kujifungua au muda wowote ambao Mamlaka ya Elimu itaona unafaa. Lakini kusimamishwa masomo kusizidi miaka miwili.

Kifungu cha 4 (3) cha Sheria hii kinaeleza kuwa mwari atakayepata ujauzito akiwa yupo katika masomo atasimamishwa masomo na anaweza kurejea katika masomo mwaka unaofuata baada ya kumaliza kuitumikia jamii au muda wowote ambao Mamlaka ya Elimu itaona

*Inaendelea Uk. 15*




***Baadhi ya kinamama wakiandamana kuashiria maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.***

# Ijue Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja

*Inatoka Uk. 14*

unafaa.

Lakini Kifungu cha 4 (4) cha Sheria ya Kuwalinda Wari na Watoto wa Mzazi Mmoja Nam. 4 ya 2005 kimeweka wazi kuwa Mamlaka ya Elimu inaweza kumzuia mwari asijiunge tena na masomo ikiwa itabaini kuwa hajajirekebisha tabia yake.

**MATUNZO YA WATOTO WA MZAZI MMOJA**

Kifungu cha 5 (1) cha Sheria hii kuwa mwari, mtoto wa kike, mwanamke aliyeachwa au mwanamke ambaye hajaolewa akipata ujauzito au akijifungua nje ya ndoa anaweza kufungua kesi ya madai katika Mahkama ya Wilaya kudai matunzo ya mtoto kutoka kwa mtu aliyedhaniwa kuwa ni baba wa mtoto au aliyemsababishia uja uzito kabla ya kujifungua au wakati wowote kabla ya mtoto hajatimiza umri wa miaka kumi na nane au kuweza kujitegemea mwenyewe.

Vile vile imeelezwa na sheria hii kwamba mtu atakayekubali kuwa ni baba wa mtoto au mhusika wa mimba hiyo kwa kauli yake au kwa vitendo vyake basi hatoruhusiwa kulikana jambo hilo na anaweza kushtakiwa kwa ajili ya kutoa matunzo isipokuwa kama atathibitisha mbele ya Mahkama kuwa yeye sio baba wa mtoto.

Hata hivyo, ifahamike kwamba ingawa mtu huyo analazimika kutoa matunzo kwa mtoto lakini mambo yote yanayohusu mirathi hayahusiani na sheria hii na badala yake yatashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria za Mirathi.

**WAJIBU WA MWARI JUU YA KUTAJA JINA LA MHUSIKA**

Ni jambo lililo wazi kuwa mwari ndiye anamjua mtu aliyempa ujauzito. Hivyo Kifungu cha 6 (1) cha Sheria hii kinasema kwamba itakuwa ni wajibu wa mwari aliyepata uja uzito kumtaja mtu aliyempa uja uzito. Ikiwa atakataa atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatakiwa kutumikia jamii kwa miezi mitatu.

Mwari au mwanamke ikiwa atatoa jina ambalo ni tofauti na la mtu anayehusika na uja uzito wake na Mahkama ikajiridhisha kuwa amefanya hivyo kwa makusudi atakuwa ametenda kosa na atalazimika kuitumikia jamii kwa miezi sita (6). Lakini mwari atakuwa na kinga ikiwa atathibitisha kuwa ujauzito ulitokana na kitendo cha kubakwa kwa kikundi, kujamiana kwa maharimu au mazingira mengine yeyote ambayo yatamfanya ashindwe kumtambua mbakaji.

**WAJIBU WA KUMTUNZA MTOTO.**

Kifungu cha 8 cha Sheria hii kinasema kuwa itakuwa ni wajibu wa baba au mtu anayedhaniwa kuwa ndiye baba wa mtoto kumtunza mtoto wake na kutoa mambo muhimu ya maisha yake kama vile mavazi, nguo, chakula, elimu,afya, makaazi mazuri na mengineyo kwa mujibu wa uwezo wake. Maana ya elimu ya elimu ya msingi kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Nam. (ngapi?) ya 1982 na ikiwa uwezo wa baba unaruhusu itazidi mpaka elimu ya juu.

**UWEZO WA MAHKAMA WA KUTOA AMRI YA KUWEKA DHAMANA (SECURITY) KWA AJILI YA MATUNZO**

Kifungu cha 10 (1) na (2) cha Sheria hii kinaeleza kuwa Mahkama inaweza ikamuamuru mtu mwenye wajibu wa kutoa matunzo kutoa nusu au sehemu yote ya kile anachotakiwa kutoa kwa kuweka mali kwa dhamana ambapo kupitia kwa mali hiyo matunzo hayo au sehemu yake yatatokana na mali hiyo. Vile vile Mahkama inaweza ikaamuru kukamatwa na kuuzwa kwa mali ya mtu atakayethibitika kuwa ana wajibu wa kutoa matunzo.

**MUDA WA AMRI YA MATUNZO YA MTOTO WA MZAZI MMOJA**

Kifungu cha 12 (1) cha Sheria hii kinaeleza kuwa amri ya matunzo itafika mwisho pindipo mambo yafuatayo yatatokea;

a) Kifo cha baba;
b) Kifo cha mtoto;
c) Mtoto akitimia umri wa miaka kumi na nane;
d) Mtoto akiweza kujitegemea kabla ya kutimiza miaka 18;
e) Pale atakapoolewa, kwa mtoto kike.

Hata hivyo imeelezwa kuwa amri ya matunzo itaendelea kuwa na nguvu kisheria kwa mtoto ambaye ametimiza miaka 18 lakini hali yake kiakili au kimwili inamzuia kuweza kujitegemea mwenyewe au mtoto bado anaendelea na masomo.

Kifungu cha 13 cha Sheria hii kinaeleza kuwa haki ya mtoto ya kupata matunzo chini ya amri ya Mahkama itasita mara mama yake atakapoana na baba yake na haki hii itarudi tena mara wanandoa hao watakapoachana na ikiwa mtoto hajaweza kujitegemea mwenyewe.

**UFUNGUAJI WA KESI YA KUDAI MATUNZO YA MTOTO**

Kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai, Sura ya 8, Sheria ya Zanzibar, kila mtu atakayefungua kesi ya madai atalazimika kulipa ada ya Mahkama itakayotegemea na dai analodai. Hata hivyo, Kifungu cha 5 (4) cha Sheria hii mdai wa shauri la matunzo ya mtoto anasameheka na hatolipa ada. Madhumuni ya Kifungu hiki ni kuwawezesha wari, watoto wa kike na wanawake watakaopata ujauzito nje ya ndoa kuweza kufungua kesi kwa urahisi.

**CHANGAMOTO**

i. Jamii kutokujua Sheria hii. Sheria ya kuwalinda Wari na Watoto ipo lakini haikutekelezwa kwa muda mrefu na kusababisha kuongezeka udhalilishaji wa wari,watoto wa kike na wanawake ambao hawajaolewa.
iii. Wazazi wengi huyamaliza masuala ya uja uzito nje ya ndoa katika ngazi ya familia.
iv. Kukosekana kwa ushirikiano sahihi kutoka kwa jamii. Baadhi ya wakati jamii inasita kutoa ushirikiano wa kutoa ushahidi.
v. Rushwa na uenyeji huathiri uendeshaji wa kesi.

**MAPENDEKEZO**

a. Taasisi za Serikali na Kiraia zitoe elimu ya Sheria hii.

Hatua za sheria zichukuliwa dhidi ya wakosaji.

**HITIMISHO**

Jamii ibadilike na kutoa ushirikiano kuhakikisha haki za wari na watoto wa mzazimmoja zinalindwa kwa gharama yoyote ile na kwa mujibu wa sheria za nchi. Lakini watendaji husika watekeleze majukumu yao kwa kuzingatia maadili ya kazi zao ipasavyo ili kulinda haki za wari na watoto wa mzazi mmoja.

# Kuingia Katika Ardhi Kwa Maudhi (*Trespass to land*)

**UTANGULIZI**

**ARDHI** ni moja katika rasilimali kuu za uzalishaji mali. Zipo sheria mbali mbali zinazosimamia matumizi ya ardhi. Pamoja na sheria hizo, hairuhusiwi kuingia katika ardhi ya mtu mwengine au nyumba bila ya ruhusa ya mmiliki (*owner*) au dhamana (*possessor*) kinyume chake anaweza kushtakiwa kuingia kwenye ardhi hiyo kwa nia ya kutenda kosa (criminal trespass) au kwa lengo la kubughudhi (*tortious trespass*). Katika makala hii Mwanasheria **JINA MWINYI WAZIRI** anaelezea kuingia katika ardhi au nyumba kwa nia ya maudhi.

**MAANA YA KUINGIA KATIKA ARDHI KWA MAUDHI**

Ni kitendo cha kuingia katika ardhi au nyumba bila ya ridhaa kinyume na sheria. Kosa hili linapatikana katika Kifungu cha 302 (1) (a-b) Sheria ya adhabu (*Penal Act No*. 6 2004) ya Zanzibar na Sheria ya Madhara (*Law of Torts*). Ikiwa kosa litafunguliwa chini ya Sheria za Uhalifu, mlalamikaji lazima athibitishe kuingia kwa nia ya kutenda kosa. Sheria ya Madhara mlalamikaji ana lengo la kulipwa fidia ikiwa Mahkama itaridhika na ushahidi.

Aidha, kuingia katika ardhi kwa maudhi ni kitendo cha mtu kuingia mwili mzima au sehemu ya mwili au kuingiza kitu katika milki au eneo la mtu mwengine bila ya ruhusa. Ni jukumu la mdai kuthibitisha kuingia kwa anayeshtakiwa katika nyumba au ardhi kwa madhumuni ya kuleta maudhi kwa mmiliki wa eneo au mdhamini wa eneo au nyumba.

**VIPENGELE VYA KUINGIA KATIKA ARDHI KWA MAUDHI**

Vipengele vya kuingia katika ardhi kwa maudhi ni hivi vifuatavyo;

1. Kuingia katika ardhi au nyumba ya mtu
2. Eneo limilikiwe au liwe chini ya dhamana ya mtu
3. Kuingiza kitu katika ardhi au nyumba bila ya ruhusa
4. Kubakia katika ardhi au nyumba baada ya muda wa ruhusa kumalizika.
5. Kukosekana kwa ruhusa kutoka kwa mmiliki au mdhamini.

**KUINGIA KATIKA ENEO LA MTU**

Kitendo cha kuingia katika ardhi au nyumba ya mtu inayomilikiwa au iliyo chini ya dhamana ya mtu mwengine au mlalamikaji. Kuingia hata kwa sehemu ya mwili bila ya ruhusa inakuwa kosa. Pia kuingia kwa lengo maalum lakini ukafanya kitu chengine itakuwa ni kosa kisheria. Mfano ni uhalali wa kutumia njia (*easement*) iliyopo ndani ya shamba au nyumba ya mtu na baadaye ukakaa au kupumzika katika shamba hilo utakuwa umefanya kosa.

Haitokuwa kosa ikiwa mtu ataingia katika ardhi ya mtu mwengine kwa kulazimishwa. Mfano, mlevi ameanguka na watu wengine wakamuokota akiwa hajitambui na kumuweka katika nyumba ya mtu bila ya ridhaa ya mhusika; hatokuwa na kosa kisheria kwa sababu hakutenda hivyo kwa ridhaa yake.

**ENEO LA MTU ANALOMILIKI KISHERIA**

Eneo linajumuisha eneo lote linalomilikiwa au lipo chini ya dhamana ya mtu ikiwemo sehemu zote zinazozunguka eneo au nyumba au juu ya anga au chini ya ardhi. Kosa litathibitika ikiwa mdai atathibitisha uhalali wa kumiliki au kudhamini eneo husika kisheria. Katika kesi ya ***JELA KALINGA V.OMARY KARONUWANA* (1991)** TLR 69, mlalamikaji alikuwa ni dhamana (possessor) wa eneo lililolalamikiwa na mlalamikiwa aliingia katika eneo bila ya ruhusa lakini alisema kwamba aliyeshtaki sio mmiliki wa eneo hilo (*owner*). Maamuzi ya kesi yalikuwa ni mwenye dhamana pia ni mmiliki kisheria hivyo mlalamikiwa ni mkosa na alitakiwa kulipa gharama zilizodaiwa na mdai.

**KUINGIZA KITU KATIKA ENEO LA MTU**

Sheria ya Madhara inatambua kuhusiana na uingizaji wa kitu chochote katika eneo la mtu bila ya ruhusa ya mmliki kuwa ni kosa na atakayebainika kutenda kosa hilo anaweza kushtakiwa na kutakiwa kulipa fidia. Mfano wa vitu ni kuzika mabomu chini ya ardhi, kuingiza bomba la maji katika ardhi ya mtu, mkono au fimbo.

**WANYAMA KUINGIA KATIKA ENEO LA MTU**

Wanyama wanaoweza kuathiri, isipokuwa, mbwa na paka, ni kosa kuingia katika ardhi au nyumba ya mtu. Katika kesi ya ***ANDERSON V. BUCKTON*** (1815) mifugo ya mlalamikiwa iliyokuwa na maradhi iliingia katika shamba na

*Inaendelea Uk. 17*



***Hairuhusiwi kuingia katika ardhi***

# Kuingia Katika Ardhi Kwa Maudhi (*Trespass to land*)

*Inatoka Uk. 16*

kuambukiza maradhi mifugo ya mlalamikaji. Mahakama ilisema kwamba mlalamikiwa ni mkosa kwa hasara zilizotokana na maradhi ya wanyama wake pamoja na majani ya shamba hilo.

**KUBAKIA KATIKA ENEO LA MTU BAADA YA RUHUSA KUMALIZKIA**

Kisheria mtu hatakiwi kubakia katika sehemu aliyoruhusiwa kukaa ikiwa muda umemalizika. Mfano, mtu kapewa kadi ya mualiko kuhudhuria shughuli kuanzia saa tatu asubuhi mpaka saa tano asubuhi. Ikiwa ataendelea kubaki katika eneo bila ya sababu ya msingi baada ya muda ulioelezwa atakuwa ametenda kosa.

**KUKOSEKANA KWA RUHUSA KUTOKA KWA MMILIKI**

Ni kosa kuingia katika eneo la mtu au liliopo chini ya dhamana ya mtu bila ya ruhusa. Lakini watu wanaofanya kazi maalum na katika mazingira maalum hawabanwi na sheria hii. Watu wa aina hii wanatakiwa kufanya kazi waliyokusudia na si vyenginevyo. Mfano Afisa wa Uhamiaji wakati wa kutekeleza kazi zake, Askari wa zima moto pale linapotokezea tatizo la moto, Askari polisi wanapotaka kufanya upekuzi na ikiwa watatimiza taratibu za kisheria na wasoma mita za umeme au maji .

**KUINGIA KATIKA ARDHI KWA NIA YA UHALIFU *(Criminal Trespass)***

Upo uwezekano wa mtu aliyefanya kosa la kuingia katika ardhi kwa maudhi kushtakiwa kwa kosa la jinai ikiwa yatatokea mazingira yafuatayo;

- Mtu aliyejenga uzio au ukuta au nyumba katika eneo la mtu mwengine bila ya ridhaa ya mmiliki akijua kwamba eneo hilo si lake.
- Mtu aliyeingia katika eneo la mtu mwengine kwa nia ya kutenda kosa la uhalifu, kwa mfano wizi wa mazao.
- Mtu aliyeingia katika eneo la mtu mwengine na kubakia kwa muda kwa makusudi na akitambua kuwa ni kosa.
- Kuingia katika eneo la mtu na kufanya kosa la uhalifu, mfano: "A" ni mmiliki wa shamba na katika eneo la shamba lake ipo njia (*easement*) iliyozoeleka kupitwa na kuna matunda, "B" alipita na kuokota matunda, "B" atakuwa amefanya kosa na anaweza kushtakiwa kwa kosa la wizi.

**FIDIA KWA MAKOSA YA KUINGIA KATIKA ENEO LA MTU**

Fidia zinazoweza kulipwa ni hizi zifuatazo:-

a) Mdaiwa atalipa gharama zinazotakiwa ikiwa ni fidia kutokana na kitendo alichokifanya .
b) Mdai kutumia nguvu zinazokubalika kukirejesha kitu kilichochukuliwa na mdaiwa kwa kumnyanganya au kwa kutumia amri ya Mahkama.
c) Mdai kuruhusiwa kukizuia kitu kilichoharibiwa mpaka alipwe fidia iliyotakiwa.

**UTETEZI DHIDI YA KUINGIA KATIKA ARDHI KWA MAUDHI**

Mlalamikiwa anaweza kujitetea ikiwa itatokezea moja ya yafuatayo;

1) Ridhaa ya mmiliki juu ya kutumia eneo au nyumba.
2) Ruhusa kwa mujibu wa sheria *(Authority by law/statutory authority).*
3) Kukiwa na ulazima wa kuingia katika eneo *(By necessity).*
4) Kuingia kwa kulazimishwa *(By force of another).*

**CHANGAMOTO ZINAZOJITOKEZA**

Changamoto zinazoweza kujitokeza katika kuingia katika ardhi kwa maudhi;

- Kutotii sheria: Watu wengi hawafuati sheria hasa sheria za madhara na badala yake hufanya mambo kwa mazoweya.
- Kukosekana kwa msukumo wa vyombo vinavyohusika. Mara nyingi makosa yanayoangaliwa ni ya jinai na makosa ya madai kutopewa uzito.


**HITIMISHO**

Sheria ya Madhara ni muhimu kufuatwa ili kuepuka maudhi katika jamii. Ni vizuri tuwajibike ili nchi ifuate Utawala wa Sheria.



*kwa maudhi (Trespass to Land)*

# Ripoti ya Haki za Binadamu Zanzibar 2010 Yazinduliwa



**JAJI** wa Mahkama Kuu Zanzibar, Mheshimiwa Abdulhakim Ameir Issa amekipongeza Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kwa kuendelea kutayarisha na kuchapisha ripoti ya Haki za Binadamu Zanzibar tokea mwaka 2006.

Akizindua ripoti ya Haki za Binadamu ya Zanzibar mwaka 2010, jaji huyo alisema juhudi za Kituo za kutayarisha ripoti lazima zipongezwe kwasababu ni kielelezo cha umakini (*seriousness*) katika kulinda Haki za Binadamu.

*"Ninafarijika kuona ripoti hii ya kila mwaka inatayarishwa bila ya kukosa tokea mwaka 2006,"* alisema Jaji huyo ambaye alishiriki kwa kutoa ushauri wa ripoti ya kwanza ya Haki za Binadamu.

Alisema utayarishaji wa ripoti ya Haki za Binadamu umeboreshwa na ripoti inajumuisha maeneo zaidi ukilinganisha na ripoti zilizopita.

Jaji Abdulhakim alisema ni wajibu wa kila mtu popote alipo kuheshimu Haki za Binadamu kwa vitendo ili kuimarisha utawala wa sheria na utawala bora nchini.

Alisema ongezeko la majaji wa Mahkama Kuu Zanzibar kutasaidia kupunguza mrundikano wa kesi jambo ambalo litachangia mchakato wa kutekeleza Haki za Binadamu. Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein aliteua majaji wanne wa Mahkama Kuu mwaka jana.

Ripoti ya Haki za Binadamu inatayarishwa kwa mashirikiano baina ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu Tanzania Bara (LHRC) na ZLSC. LHRC inatayarisha ripoti ya Haki za Binadamu kwa upande wa Tanzania Bara na ZLSC inatayarisha ripoti kwa upande wa Zanzibar.

Akitoa muhtasari wa ripoti ya Haki za Binadamu ya mwaka 2010, Afisa wa Mipango wa ZLSC, Bi Harusi Miraji, alisema Haki za Binadamu zinaheshimiwa katika baadhi ya sekta lakini pia zinavunjwa katika sekta nyengine.

Kwa mfano, alisema sekta ya sheria na siasa zimepiga hatua katika kuheshimu Haki za Binadamu Zanzibar lakini alisema bado kuna changamoto katika taasisi za Polisi, Mahkama na Ajira .

Alisema rushwa imeshamiri katika baadhi ya sekta hapa Zanzibar na viwango vya mishahara ni vidogo kwa wafanyakazi kwa kujikimu katika mahitaji muhimu.

Uzinduzi wa ripoti ya Haki za Binadamu ya 2010 ulifanyika katika ukumbi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) na kuhudhuriwa na wageni mbali mbali.

# Magereza Yatenganishe Wafungwa Watoto Na Watu Wazima - Wito

**UONGOZI** wa Vyuo vya Mafunzo Zanzibar umeombwa kuwatenganisha watoto na wafungwa watu wazima ili kutekeleza Mikataba ya Kimataifa inayolinda haki za watoto.

Wito huo umetolewa katika semina waliyofanyiwa maafisa wa Vyuo vya Mafunzo Unguja na Pemba ili kuwaelimisha haki za watoto. Semina hiyo ya siku mbili iliandaliwa na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar kwa kushirikiana na Save the Children.

Wataalamu mbali mbali waliowasilisha mada za haki za watoto walisisitiza kwamba kuwachanganya watoto na watu wazima katika magereza ni kinyume na Mkataba wa Watoto wa Kimataifa (CRC) na Mkataba wa Afrika wa Watoto (ACWRC).

Walieleza kwamba watoto wataathirika kitabia na kisaikolojia na inaweza kusababisha kuwa wakorofi zaidi watakapomaliza vifungo vyao ikiwa watachanganywa na wafungwa watu wazima.

*"Watoto watajifunza tabia mbaya na mbinu za uhalifu kutoka kwa wafungwa watu wazima,"* walisema wataalamu wa sheria waliowasilisha mada.

Aidha, walisema kwamba kuchanganywa kwa wafungwa watu wazima na watoto kutasababisha watoto kuingiliwa kinyume na maumbile.

Vile vile, uongozi wa Vyuo vya Mafunzo umeshauriwa kubuni njia bora ya kuwasomesha watoto waliofungwa ili wapate haki ya elimu. *"Inawezekana muda wa mtoto wa kusoma kupita ikiwa atawekwa gerezani kwa hiyo bora wasomeshwe wakiwa ndani ya gereza"* walisema wataalamu.

Wakichangia mada, maafisa wa Vyuo vya Mafunzo walisema kwamba hali ya magereza Zanzibar imeimarishwa ikilinganishwa na miaka iliyopita.

*"Tunajitahidi kuboresha hali ya magereza yetu lakini tatizo kubwa ni bajeti finyu tunayopewa na Serikali,"* walisema.

Walisema mipango ya maendeleo ya kuwasaidia wafungwa imetayarishwa lakini inakwama kwa ukosefu wa fedha.

# Kamati ya Sheria ya BLW yatembelea ZLSC

**KAMATI** ya Sheria na Katiba ya Baraza la Wawakilishi (BLW) Zanzibar imetembelea Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kiliopo Migombani, Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi.

Ziara ya Kamati iliyofanyika hivi karibuni ni ya kwanza tokea Kituo kilipoanzishwa mwaka 1992.

Mkurugenzi wa Kituo , Bw. Iss-Haq Ismail Shariff aliielezea ziara ya wajumbe wa Kamati hiyo kwamba imefungua ukurasa mpya wa mashirikiano baina ya chombo cha kutunga Sheria na Asasi za kiraia.

*"Tumefurahi kwa waheshimiwa kututembelea ili kujua tunachofanya na mipango yetu ya kueneza elimu na kutoa msaada wa sheria Zanzibar,"* alisema Mkurugenzi huyo.

Alisema Kituo kimeanzishwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wote wa Zanzibar kufahamu sheria na kupewa msaada wa sheria wanapofikwa na matatizo.

Katika utendaji kazi, alisema Kituo kinaongozwa na maadili ya taaluma ya sheria na hakijafungamana na chama chochote cha siasa.

Naye, kiongozi wa msafara Mheshimiwa Bi. Panya Ali Abdalla , Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Katiba wa Baraza la Wawakilishi, alisema wamefarijika na kazi zinazofanywa na Kituo na kuahidi kushirikiana bega kwa bega kwa maslahi ya umma.

Alisema ziara hiyo imewafungua macho na kuahidi kuwa mabalozi wazuri wa kueleza malengo na mafanikio ya Kituo.

Wajumbe wengine waliokuwemo katika ziara hiyo ni Waheshimiwa Rajab Khatib, Mussa Ali Hassan na Suleiman Hemed Khamis. Pia walikuwemo Makatibu wa Kamati Bi. Nassra Awadh na Bwana Abubakar Iddi.

Waasisi wa Kituo ni marehemu Profesa Haroub Miraji Othman, mwanasheria mkongwe Maalim Hassan Said na mwanasheria Bi Fatma Maghimbi.

Afisi Kuu ya Kituo ipo Zanzibar katika eneo la Migombani na afisi ndogo ipo Pemba katika eneo la Chakechake.

Kituo kimeweka wasaidizi wake wa sheria (*paralegals*) katika majimbo yote 50 ya uchaguzi yaliyopo Zanzibar kwa madhumuni ya kusogeza huduma karibu na wananchi.

# Mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto (1999)



*Watoto wakiwa wanafuria jambo*

***Jarida la Sheria na Haki linaendelea kuchapisha mkataba wa Afrika wa Haki na Ustawi wa Mtoto wa mwaka 1990 kwa madhumuni ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu haki za mtoto.***

Serikali inapaswa kuwasaidia wazazi au walezi wako kukutunza.

**Kipengele cha 21**
Una haki kulindwa dhidi ya mila na desturi zenye ubaguzi wa kijinsia au zinazoathiri afya na maisha yako.

Ndoa zote zitaandikishwa na haitaruhusiwa mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18 kuoa, kuolewa au kuwekewa ahadi ya kuoa au kuolewa na na mtu yeyote.

**Kipengele cha 22**
Una haki ya kulindwa wakati wa vita na kuepushwa na athari zake.Pia una haki ya kulindwa dhidi ya kujiunga na jeshi au kushiriki katika vita.

**Kipengele cha 23**
Una haki ya ulinzi maalum na msaada kama wewe ni mkimbizi. Mkimbizi ni mtu yeyote ambaye amelazimika kuondoka nchini kwake kwa sababu sio salama.

**Kipengele cha 24**
Iwapo itashindikana kuishi na wazazi wako, una haki ya kuishi na walezi, wazazi wa kufikia au katika vituo vya kutunzia watoto.

Iwapo itabidi uishi na walezi hawa nchi tofauti na uliyozaliwa, una haki ya malezi yako kufuata sheria za nchini kwenu.

**Kipengele cha 25**
Iwapo unaishi mbali na wazazi ,una haki ya:-

**a.** kutunzwa na watu wengine.
**b.** Kuunganishwa nao tena nafasi ikijitokeza.
**c.** Kutunzwa kwa namna ambayo itaendeleza malezi yako kwa kufuata kabila, dini na lugha yako ya kuzaliwa.

**Kipengele cha 26**
Una haki ya kulindwa dhidi ya kubaguliwa iwapo unaishi katika nchi ambako kuna ubaguzi wa rangi.

**Kipengele cha 27**
Una haki ya kulindwa dhidi ya udhalilishaji wa kijinsia na kushirikishwa na picha, filamu au maandishi ya ngono.

**Kipengele cha 28**
Una haki ya kulindwa dhidi ya dawa hatari za kulevya

**Kipengele cha 29**
Una haki ya kulindwa dhidi ya kutekwa nyara, kupelekwa sehemu usiyotaka au kuuzwa. Hii pia inahusisha kulindwa dhidi ya kutumiwa kuomba omba mitaani au kwingineko.

**Kipengele cha 30**
Kama bado unahitaji malezi ya karibu ya mama na anashitakiwa mahakamani, una haki ya;

**a.** adhabu nyingine zizingatiwe kabla ya kifungo.
**b.** ya kutofungwa naye iwapo , atahukumiwa kifungo.
**c.** asihukumiwe kifo.

**Kipengele cha 31**
Kwa kadiri ya umri na uwezo wako, una wajibu wa;

**a.** kuulinda umoja wa familia yako, kuwaheshimu wazazi na wakubwa wako na kuwasaidia wakati wa shida.
**b.** kulinda na kudumisha mila na desturi za kiafrika na moyo wa kuvumilia watu na mawazo tofauti na yako.
**c.** kulitumikia taifa lako kwa akili na nguvu zako zote, ukienzi umoja na mshikamano wake.

**Vipengele vya 32 hadi 48**
Vipengele hivi huelezea jinsi serikali za mataifa na mashirikia yasiyo ya kiserikali yatakavyofanya kazi kuwahakikishia watoto haki zao.

Hii sio tafsiri rasmi ya mkataba huu ila umerahisishwa ili uweze kueleweka na watu wengi wakiwemo watoto.

Hadi tarehe I Aprili 2005, nchi 33 wanachama wa Muungano wa Afrika zilikuwa zimeridhia mkataba huu. Kuuridhia mkataba maana yake ni kukubali kuutekeleza.

Jamhuri ya Muungano ya Tanzania iliridhia mkataba huu tarehe
16 Machi 2003.

Tanzania inaandaa ripoti ya kwanza ya utekelezaji itakayoiwasilisha kwa Kamati ya Muungano wa Afrika inayosimamia mkataba

**Save the Children (UK)**
**Ofisi ya Tanzania**
**S.L.P 10414,**
**Simu 2701725**
**Dar es Salaam**
**Tupo Msasani kiwanja namba 84, Barabara ya zamani ya Bagamoyo nyuma ya ofisi za TANESCO**

Save the Children

**P.O.Box 1267, 2nd Floor, Tiger House**
**Majestic Cinema/Vuga Street.**
**Zanzibar, Tanzania**
***www.savethechildren.org.uk***

Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

# SHERIA NA HAKI

*Kwa kila Mwananchi*

Ifanye haki Iwe shauku

Toleo Na. 006 | Jarida la kila miezi mitatu | Aprili - Juni, 2011

# ZLSC yawapongeza JM na MM Zanzibar

KITUO cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kimempongeza Jaji Mkuu (JM) mpya wa Zanzibar, Mheshimiwa Omar Makungu na Mwanasheria Mkuu (MM) mpya wa Zanzibar Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kuteuliwa kushika nyadhifa hizo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya ZLSC Profesa Chris Maina Peter alisema Mheshimiwa Makungu na Mheshimiwa Othman ni wataalamu wa sheria waliobobea na wametumia muda mrefu wa maisha yao katika fani ya sheria.

"Ninawafahamu vizuri waheshimiwa hawa. Tumeshirikiana sana kuendeleza fani ya sheria Zanzibar. Tunawapa hongera na kuwatakia kila la kheri katika nyadhifa zao hizo," alisema Profesa Peter hivi karibuni.

Kabla ya kuteuliwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Makungu alikuwa Kaimu Jaji Mkuu wa Zanzibar. Aliwahi kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar. Aidha, Mheshimiwa Makungu alikuwa Makamo Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa (NEC) na kuwa mjumbe wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

Vile vile alikuwa mwanasheria wa Serikali katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa muda mrefu. Mheshimiwa Makungu anachukua nafasi iliyokuwa wazi baada ya aliyekuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar, Mheshimiwa Hamid Mahmoud Hamid kumaliza mkataba wake.



Jaji Mkuu:
Omar Makungu



Mwanasheria Mkuu:
Othman Masoud Othman

Baada ya kustaafu kwa hiyari, Mheshimiwa Hamid aliendelea kuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar kwa mkataba.

Mheshimiwa Othman, kabla ya kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar alikuwa Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar. Aidha aliwahi kuwa Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu Mkuu katika Wizara ya Katiba na Utawala Bora. Vile vile alikuwa mwanasheria wa Serikali katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa muda mrefu.

Profesa Peter alisema ZLSC itashirikiana nao katika kuendeleza fani ya sheria Zanzibar.

"Sote ni wadau wa sekta ya Sheria na mashirikiano ni muhimu kuendeleza sekta yetu" alisema Profesa.

Alisema baadhi ya maneno ya mashirikiano ni utayarishaji wa Ripoti Sheria ya Zanzibar.

Profesa alisema utayarishaji na uchapishaji wa Ripoti ya Sheria ya Zanzibar umesita kwa muda mrefu, kwa sababu tofauti ikiwemo mfumo wa Sheria kubadilika.

## Wanawake waloachwa, ulezi wasaidiwe

Wanawake wateseka, Mizigo wanaachiwa.
Wakishapewa talaka, Watoto wakumbiziwa.
Kwa ulezi wateseka, Wakosa kusaidiwa.
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

Kinamama wateseka, Kuhudumia watoto.
Kuchwa wanahangaika, Maisha kwao mazito.
Watafuta cha kupika, Wakawalishe watoto.
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

Wanatupiwa Ulezi, Halafu wanakimbiwa.
Mababa hawaulizi, Si kwa chai wala dawa.
Huduma na makaazi, Zote mama aachiwa!
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

Watoto wao walishe, Nani tawasaidia?
Na skuli wasomeshe, Ni vipi watalipia?
Nguo pia wawavishe, Ni wapi watazitoa?
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

Watoto wataka soma, Afya nayo wapatiwe.
Ameshatupiwa mama, Kila kitu anunuwe.
Tuwaonee huruma, Mashaka wasaidiwe.
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

Mama yu kwenye kikiri, Ya watoto kuwalisha.
Baba hapati khabari, Ala raha za maisha!
Asubirilo mahari, Na siku ya kuozesha.
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

Wanawake taabani, Zimedhofu hali zao.
Kuchwa wamo majiani, Wafukuzia chajio.
Wanateseka kwa nini, Wamezaa peke yao?!
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

Wamekosa pa kushika, Wanawake wateseka.
Ulezi umewashika, Taabani wamechoka.
Msaada wanataka, Wapate kupumzika.
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

Ulezi wasaidiwe, Wasiachwe peke yao.
Watoto waangaliwe, Kwenye mahitaji yao.
Huduma nawapatiwe, Kutoka kwa baba zao.
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

Jamii naiamke, Kinamama kuokowa.
Dhiki kwao iondoke, Ulezi kusaidiwa.
Wazazi wajumuike, Sio pweke kuachiwa.
**Wanawake waloachwa, Ulezi wasaidiwe.**

**SAID RASHID HASSAN**
**ZLSC – PEMBA.**